

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

Verbatim Report Of

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, COAST
PROVINCE, HELD AT KISAUNI BALUCHI HALL.**

ON

7TH OCTOBER 2002

DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL – COAST PROVINCE HELD AT KISAUNI BALUCHI HALL ON MONDAY 7TH OCTOBER 2002

Present:

Com. Prof A.I. Salim

Secretariat Staff in Attendance

William Opili - Assistant Programme Officer.
Gladys Osimbo - Verbatim Recorder

Others

District Co-ordinator Sylvia Chidodo
District Cordinator Ahmmed Mohamed
Assistant D. Co-ordinator
Sheha Shamisi

The meeting started with at 10.15 am.

Com. Prof. Salim: Salaam Aleykum? Hamjambo nyote? Tafadhalini wale wajamaa waliosimama wakae tuanze, maana tuna marathon session, mkutano mrefu kidogo na tungenda kumaliza kabla ya saa (**inaudible**). Pia kabla ya kuanza ningomba mmoja wetu aje atufungulie mkutano kwa dua. Tafadhalini mmoja wenu aje hapa mbele tufungue mkutano. Any volunteers or volunteer? Tafadhali.

Sheikh Ali: Arabic dialect:

Translator

Sheikh Ali: Yarabi tujalie mkutano huu, mkutano mwema. Tujalie mkutano huu Yarabi utupe faidha na ulete makusidio iliyo kusudiwa. Yarabi jalia hii tume ifaulu, na Katiba hii ipite na iende Mwenyezi Mungu. Lipe nguvu Yarabi na utupe nguvu sisi wenye kuisemea na kuitetea. Utupe nguvu kuitetea na mpaka ipite.

Sheikh Ali: Arabic dialect:

Translator:

Com. Prof. Salim: Shukran Sheikh. Ningependa kwanza kuwashukuru nyote kwa kufika hivi leo katika mkutano huu. Na tunataraji vile tutaendelea jamaa wengine watafika kuongeza idadi ya watu katika mkutano huu ambayo, bila shaka sote twakubali kwamba ni mkutano muhimu sana. Lakini kabla kuendelea mbele ningependa kuwajulisha hawa wenzetu waliokuwa hapa kunisaidia katika kuendesha mkutano huu. Kwa upande wangu wa kulia yuko bwana Ahmed ambaye bila shaka nyote mwamjua – District co-ordinator Mombasa. Upande wangu wa kushoto ni mwenzake Silvia ambaye amekuwa kwa muda mrefu sasa akitusaidia katika kusambazisha, kuhamasisha watu kuhudhuria mikutano, na kutayarisha mikutano hiyo ifanyike kwa njia ambayo yafaa. Naal hamdulilhai amefaulu katika kazi hiyo. Pale wako wenzangu pia vijana, ni William, na Gladys, hayo kazi yao pia ni muhimu sana kuhakikisha kwamba yote ambayo yatasemwa, yatanaswa, na pia kwamba wataweka recodi au minutes ya mkutano huu ili tukirudi tutoe pia repoti yetu tukiwa kikundi kimoja cha wale ambayo wameshugulikia areas hizi za Pwani.

Mathumuni ya mkutano huu kwa hakika ni kuwaeleza juu ya mswada wa Katiba mpya ambayo tume imetayarisha. Na pia juu ya repoti ndogo ya kazi zetu. Nafikiri mumepata kusikia jinsi ambavyo tumekamilisha report. Tukakamilisha mswada wa Katiba katika muda ambayo ni wa recodi, maana tumekuwa katika pressure kubwa ili tumalize haraka na Mungu akipenda tuweze kuwa na Constitution hii, itumiwe kwa uchaguzi wa mwaka huu. Jambo ambalo kwa hakika ya wezekana lakini kuna mambo mengine ya kisiasa ambayo hatuwezi kuyaingilia na kwa hivyo letu ni kuomba tu kwamba itawezekana. Sitaki kupoteza wakati kwa hakika kueleza jinsi ambavyo tumefikia kiwango hiki cha kazi yetu. Nafikiri nyote mwafahamu, jinsi tulivyoanza, jinsi tulivyoanza kutembelea kila Province, tukaeleza kazi yetu kama Tume.

Jinsi ambavyo tumeweka agents wetu, district co-ordinators kila mahali, kila district ya Kenya. Jinsi ambavyo tulipeleka Civic Education providers kuwafahamisha wananchi juu ya Katiba iliyoko hivi sasa, na zaidi ya hivyo kuwaelimisha juu ya masala na maswali muhimu katika kila Katiba, na kupata kuwatayarisha ili kupokea maoni yao. Kisha tukapata tena safari zetu tukaenea kila sehemu ya Kenya, kukusanya maoni ya wananchi, haya maswala na maswali tafauti kuhusu Katiba. Baada ya hapo tukaanza kufanya kuchungua, kusoma, kuanalyze maoni ya wananchi, maoni ya mtu binafsi, maoni ya vyama tafauti, tafauti hapa nchini. Na tukaweka watu maalum wataalam maalum kuanalyze, kuchambua yaliomo katika maoni ya wananchi, mpaka tukafika hadi ya kuandika repoti yetu juu ya kazi yetu. Na pili mswada wa Constitution.

Repoti hii kwa hakika ni repoti fupi tu, (a short version) ya kazi yetu. Utakuwa na repoti kubwa zaidi ya volume tano, ambayo

hivi sasa yaendelea kutayarishwa na Mungu akipenda hivi karibuni itakamilishwa. Na katika ripoti hii tumeleza ile kazi yetu, tukaeleza maswala muhimu yalioko ambayo tulishugulikia na pili jinsi ambavyo tulifanya kazi yetu kukusanya habari. Wananchi walituambia kitu gani, ikiwa kila swala mutaona hapo sehemu kadha wa kadha tukaeleza jinsi ambavyo swala hili tulieleza umuhimu wake kisha tukasema kwamba wananchi walituambia tufanye hivi, tufanye vile, mkifanya vile kuhusu jambo hilo. Kwa maelezo ya kazi yetu yako katika repoti au tarifa lakini kutokana na maoni ya wananchi, tukaandika mswada wa Katiba. Tuna copies chache tu ya ripoti hii fupi au taarifa hii fupi. Lakikini inshalah tutachapisha copies zingine, au nakala nyingine ili kueleza kati ya leo na conference itakayo fanyika baadaye.

Pia kwa wale ambayo wana nafasi, ningewaambia waweze kufika katika ofisi yao hapa (**inaudible**) public library, na pale wana copies za kutosha ikiwa mtu ana saa, saa mbili aweza kuja pale, aweza akasoma, akafahamu yaliyomo katika reporti na pia yaliyomo kwa tafsiri katika hii Constitution. Ingawa Constitution au mswada wa Constitution ilichapishwa katika Nation na Standard, na wale walionunua Nation na Standard siku hiyo bila shaka waliweza kuhifadhi nakala zao za hii Constitution. Sasa kukatokea ni kwamba tuna siku thelathini kuazia tarehe ishirini na saba mwezi wa September kueneza, kusambazisha yaliyomo katika report. Na mswada Constitution wananchi wapate kusoma, watapata kufahamu, na waweze kutupa feed back, watueleze wamekubali yaliyomo, hawakubali, hawakukubali, haukubali, na ni mambo gani ambayo hukufurahia nayo. Na wataka mabadiliko gani yafanywe. In other words tuko pia katika hali ya kupokea maoni sasa.

Lakini maoni tunataka sasa ni juu ya repoti au taarifa na juu ya mswada wa Constitution. Maana tukumbuke kwamba hii si Constitution. Huu ni mswada wa Constitution, draft, mapendekezo tu. Baada ya mwezi mmoja kupita ya wananchi kujadiliana juu yake, kusikiza vipindi, kusoma kwenye magazetti, na kusikiza kwetu sisi wanatume. Kisha kina Silvy na Ahmed hapa na committee yao, Constituency Constitutional Committees, kila upande wa Kenya watahugulika na mikutano kutayarisha mikutano kama hii. Kueleza wananchi zaidi juu ya Constitution. Kwa hivyo tuna mwezi mmoja kufanya kazi hii.

Baada ya hapo kutakuwa na ule mkutano mkubwa, National Constitutional Conference ambapo kutakuwa na zaidi ya wajumbe mia sita. Waakilishi na wajumbe mia sita. Utakuwa na MP's wote (WaBunge wote), pamoja na wale nominated MP's, Commissioners wote, sisi Commissioners tutatayarisha mkutano lakini hatuna vote. Nikusikiza, take notes, na kufanya kutumikia Conference. Kisha kutakuwa na waakilishi watatu kutoka kila District. Kwa mfano hapa Mombasa naona kuna waakilishi wawili, iko Bwana Faruk, na nani mwingine? Councillor (**inaudible**) na Bi Amina hajafika, hayo ndiyo watatu. Kila district ni watatu.

Kisha kutakuwa na waakilishi wa vyama vya kidini, kila aina ya dini, wakristu, waislamu, wahindu, na kadhalika. Kisha kutakuwa na waakilishi wa vikundi maalum kama walemavu na kadhalika. Ili kuhakikisha kwamba mkutano huu ukijadiliana juu ya mswada wetu wa Katiba, kutakuwemo watu ambayo wakilisha kila sehemu au sector ya wananchi wa Kenya. Ili kwamba wakikata shauri juu yake na Mungu akipenda watakubaliana hii Constitution itumiwe iwe ndiyo Katiba yetu mpya. Itakuwa ni vote of confidence kutoka kila sehemu ya wananchi wa Kenya. Watu wa dini makabila tafauti tafauti, dini tafauti

tafauti, sehemu tafauti tafauti, akina mama pia watakuwa na waakilishi wao kwa wingi nakadhalika. Hii ndiyo itakuwa National conference itaendelea kwa muda wa mwezi mmoja, na tutataraji kwamba katika muda huo kutatokea ijumaa, mafkiana, makubaliano kwamba hii Constitution ipitishwe. Na Conference ikipitisha mswada wa Katiba utapelekwa Bungeni, Bunge litapitisha maana waBunge hawatachukua muda mrefu, maana watakuwako katika hiyo conference. Watashiriki katika hiyo consensus ya Conference kupitisha mswada wa Constitution. Nafikiri tumefahamiana hapo.

Kwa hivyo jambo nitakalo lifanya hivi leo, na naomba subra yenu, nitaeleza mambo yaliomuhimu katika kila sura ya Constitution ili tuifahamu vizuri. Na baadaye inshaala tutakuwa tukipokea maoni yenu, maswali yenu, baada ya hapo. Tumesikizana juu ya procedure hiyo? Bismillahi. Mswada wa Katiba hii, unanza na kitangulizi, Preamble. Katika kuzunguka kupokea maoni ya wananchi tumepata au tumepata mapendekezo mengi sana juu ya Preamble. Katiba tuliyonayo hivi sasa haina Preamble, kitambulizi. Kitangulizi ni hasa katika Katiba umuhimu wake ni kwamba imewapa wananchi wa inchi hiyo mwelekezo. Inawapa wananchi tuseme ndoto nzuri ya jinsi ambavyo wangependa inchi yao iendelee.

Preamble hii inasema, we the people of Kenya, hiyo ni phrase muhimu sana. We the people of Kenya (sisi wananchi wa Kenya, watu wa Kenya) kwa nini watu wa Kenya? Kwa nini tuanze kabisa na watu wa Kenya? Kwa kuwa tumeambiwa katika Tume yetu muhimu ni kwamba watu ndiyo ambayo watakata shauri juu ya Katiba watakayo. It is a people driven Constitution and that is why we emphasize the people, umma, umma ndiyo sehemu muhimu katika inchi yetu. We the people of Kenya aware of our ethnic, cultural and religious diversity and determined to live in peace and unity as one indivisible sovereign nation, committed to nurturing and protecting the well being of the individual the family, and the community within our nation recognising the aspirations of our women and men for a Government based on the essential values of freedom, democracy, social justice and the rule of law exercising our sovereign and inalienable rights to determine the form of Governance of our country, and having fully participated in the Constitution making process, do adapt and give to ourselves and to our future generations this Constitution, God bless Kenya.

Utaona kwamba the people are the centre of this Constitution. The people have the aspirations, the people determine the aspirations. Ni watu ambayo wanakata shauri, wanataka mukstabal wa aina gani, mukstabal ambayo msingi wake ni kitu gani. Nafikiri sina haja kueleza zaidi ya hivo. Sawa?

Sovereignty: Exercising our sovereign and inalienable right. Sovereignty ni siada kwa kiarabu, ufalme. Uwezo wa yule ambaye ana uwezo juu ya sehemu yeyote au mtu yeyote mwingine. Hapa therefore the people are the sovereign. Na kutoka Preamble ukiendelea chapter one or sura ya kwanza utaona sura ya kwanza au chapter ya kwanza inasema sovereignty of the people and supremacy of the Constitution. Ufalme wa watu, mamlaka ya watu. Na chapter hii au sura hii inazungumza juu ya sovereignty of the people kama nilivyo sema. Ufalme wa watu, watu ndiyo ambayo wanakata shauri juu ya maisha yao na jinsi ambavo wanataka kujitawala au watawaliwe na wengine, na wale ambayo watahika zimam au reins of power are not ruling the people. They are serving the people, that is the big difference. As I will explain later on.

Supremacy of the Constitution: Katiba ndiyo itakayo kuwa sheria kubwa ya nchi. Hakuna sheria iliyo kubwa zaidi ya hivyo. Na kila kazi itakayo fanywa na mfanyi kazi wowote wa nchi. Tangu Rais mapaka yule officer mdogo, the Judicial officer yeyote au administrative officer yeyote, wote wale watafanya kazi yao kufuatia Katiba. Yeyote kati yetu ambayo anaona kwamba kazi hii inafanywa kinyume cha Katiba basi mfanyi kazi huyo aweza kuwa amevunja sheria, anaweza kushtakiwa. Hiyo ni chapter ya kwanza. Sina haja kuisoma lakini nitahighlight one or two things.

All sovereign authority belongs to the people of Kenya and may be exercised only in accordance with the Constitution. The people shall exercise their sovereign power either directly, hayo wenyewe or through their democratically elected representatives. Yaani ikiwa watu wenyewe hawawezi kushughulikia kazi hiyo, watawakilisha watu kwa shuhuli hii, kama waBunge. Hayo kazi yao ni kuwakilisha wananchi, kuwafanyia kazi yao. Na kama tutakavyo ona baadaye: ikiwa mBunge hatafanya ile kazi inavyo takikana watu wanaweza kumtoa. Ni kama mtu kumkodisha kazi, kumuandikisha kazi. Watu mwishowe wanaweza kumuondoa yeyote kati yao.

Pili: Supremacy of the Constitution: Katiba ndiyo kanuni au sheria kubwa kabisa katika nchi hii. Kenya is founded on the Supremacy of the Constitution and the rule of law and shall be governed in accordance with the Constitution. The Constitution is the Supreme law and binds all authorities and persons throughout the republic. The validity, legality, usheria au ukanuni wa Constitution hauwezi kufanyiwa challenge na mtu yeyote. Mtu yoyote hawezi kusema hii Constitution haina nguvu kufanya hivi au vile. Mtu yeyote, na nikisema yeyote I mean no one. The validity, legality of procedure of enactment or promulgation of this Constitution is not subject to challenge by or before any court, organ or agency of the State. Hakuna mtu ambayo aweza kwenda kotini akasema hii Constitution imekosea hapa. Na kanuni yeyote, au sheria yeyote nyingine ikiwa haiambatani na Katiba basi sheria hiyo ni **(inaudible)**, it is invalid. Any law that is inconsistent with the Constitution is an invalid law. Lakini muhimu ni kwamba hii Constitution itafsiriwe kwa njia ambayo itaendesha masilaha ya wananchi. It shall be interpreted in a way that promotes the values of good governance. Si nafikiri hapo chapter one nime highlight kutosha kuhusu chapter hiyo.

Chapter ya pili, inaitwa the Republic. Declaration of the Republic, Jamhuri ya Kenya. Katika sheria ile tuko nayo hivi sasa kuna mstari mmoja tu mfupi ambayo wasema kwamba Kenya ni Republic, ni Jamhuri. Lakini katika Katiba hii mpya tumeeleza kinaganaga Jamhuri ni kitu gani? What is a Republic? Lazima tufahamu, tukiitwa sisi ni Jamhuri ya Kenya, maana yake nini Jamhuri. Jamhuri ya au neno la Jamhuri limetokana na neno la Kiarabu. Jamhuri ni watu. Hata neno la kiingereza Republic, ni watu pia, jumla ya watu wanaoishi katika nchi, wanaitwa ni public. Republic ni nchi ambayo inhukumiwa na watu wake wenyewe ndiyo wamekata shauri aina gani ya Serikali wanataka iendeshe kazi yake.

The Republic of Kenya is founded on Republican principles. Jamhuri ya Kenya imewekwa msingi wake ni Republican principles. Ada au kanuni za kijamhuri. Kanuni hizo ni nini? Good governance. Kumekuwa na Republic zamani tangu siku za wa Greek, kama siku za uislaamu kujua na kila kitu. Magreek utaona kwamba do yao ilikuwa ni Republic pia, ambapo watu

wenyewe waliendesha kazi ya nchi yao. Good governance, utawala mzuri. So multi-party democracy. Democracia ambayo ni ya vyama vya kisiasa vingi. Participatory Governance, maanaka utawala ambamo watu wanashiriki katika utawala huu. Sikuwa wamewekwa kando na watu wachache ndiyo wanaendesha mambo bila kushauriana na watu.

Participatory Governance, watu wenyewe wanashiriki katika Serikali hiyo. Transparency and accountability, Serikali ambayo ni wazi unaweza kuona mambo yanavyo endelea, na ikiwa mambo yana kwenda kombo unaweza kuona mambo yanakwenda kombo. Accountability, yaani Serikali ambayo inaweka hesabu. Wananchi wanaweza kuifanyia hesabu. Kama ambavyo mwenyezi Mungu atatufanyia hesabu, wananchi pia wanaweza kufanyia Serikali hesabu. Transparency and accountability. Vipi mali ya uma inatumiwa? Accounts ziko wapi? Accounts zinatolewa kwa njia ambayo ni regular na kadhalika. Na ambapo pia kuna respect for Human Rights, Fundamental Freedom and the Rule of Law. Hiyo ni Serikali ya kijamhuri, Republican Government. Kenya is a Sovereign Republic. Tukiambiwa kwamba sisi ni Republic tunataraji kwamba Serikali yetu itawekwa juu ya misingi hii niliyo taja.

Pia chapter 3, tunazugumzia National goals, values and principles. Jambo muhimu sana. Ni kama tuseme club ya mpira au club ya kazi yoyote watakuwa na goals and principles zao jinsi ya kuendesha club ile. Basi nchi ni kama vile vile, nchi haiinuki tu ikaendeshwa ovyo. Lazima iwe na shabaha zake. Tunakwenda wapi?

Values, maadili: tunathamini kitu gani katika jamii yetu sisi? Thamani gani tunazo? Maadili katika neno la Kiswahili. Kenyan values and principles ziwe kanuni au kaida. Ni kitu gani ambacho sisi tunataka kiwekwe katika nchi yetu? Hapa tungetaja machache.

The Republic shall recognize the diversity of its people and promote the cultures of its communities. Hapo mwanzo tulisititisa umoja wa nchi. Umoja wa nchi yetu ya Kenya lazima ubakie. Katika desturi yeyote nchi lazima ibakie iwe ni moja. Lakini wakati huo huo inchi ambayo itatambua tafauti ziliyoko katika dini, tafauti zilioko katika utamaduni na kadhalika. Na kufanya kila jambo kuhifadhi kila aina ya utamaduni katika nchi hiyo. In other words diversity of cultures within the Unity of the State itatambulikana. Hiyo ni value moja na shabaha moja ya nchi yetu. The Republic shall ensure open and transparent Government and the accountability of State officials and Public Authorities, kama nilivyo sema hapo awali. Jamhuri itahakikisha kwamba Serikali yetu itakuwa ni transparent. Unaweza kuona ndani yake, it is not closed, haikufungiwa ikawa mmoja wetu hajui inafanyika nini? Katika treasury, kunafanyika nini? Hapa katika ofisi ile na kadhalika. Na iwe ofisi ile au wizara ile ni wazi, report zake zinajulikana, kazi yake inajulikana.

The Republic shall ensure access of the people to independent, impartial, and competent institutions of justice. Serikali ihakikishe kwamba watu wanaweza kufika ofisi yoyote bila taabu. Mtu ana taabu, ana mashaka yake hajui aende wapi, akienda hapa anaambiwa si hapa, ikawa mwishowe tatizo lake au mushkli wake haupati nafasi ya kufikiria yule mtu au ile ofisi ambayo itaweza kumsaidia. Kwa hivyo tutaunda Serikali ambapo mtu anaweza kufikishwa, akuambie tatizo lako lifikishwe

mahali fulani. Utakwenda sema kule, utamwona mtu fulani, anaitwa fulani, utaweza kumzungumzia juu ya shida yako. Kwa mfano kutakuwa na Public defender, Mlizi wa uma. Ofisi yake itakuwa kati ya njia nyingi sana ya mtu kwenda kushitaki akapata kuelezwa jinsi ambavyo shitaka lake litazingatiwa na khathalika.

Shabaha muhimu, lengo muhimu: the Republic shall be committed to social justice. Jamhuri italazimika kuweka uwadhilifu wa kijamii. Kutakuwa na uwadhilifu wa kijamii. Yaani mtu ahisi kwamba aishi kati ya watu ambayo wazingatia hali yake na tatizo lake. Kwa njia gani? Through appropriate policies and measures. Kutakuwa na siasa na hatua zitakazo chukuliwa kuhakikisha kwamba Wakenya wote watapata chakula cha kutosha. The basic needs for food, makao, shelter, clean water, maji masafi, sanitation, njia ya kuishi katika hali iliyo safi, elimu, matibabu na mazingara yaliyo safi, pia amani. Amani yake ita... Hilo ndilo shabaha kubwa ambalo jamhuri ya Kenya lazima watu wake wapiganie wapate haki kama hizi, ambazo haki, hizo zikipatikana kutakuwa na uwadhilifu wa kijamii katika nchi yetu ya Kenya.

Sehemu muhimu nyingine, lengo la kumi na tano au shabaha ya kumi na tano. The Republic shall promote equitable development. Jamhuri yetu ya Kenya itaeneza maendeleo au ustawi ambayo utafika kila eneo la nchi. Sikatika sehemu maalum tu. Equitable development, kuna mashtaka kwamba sehemu fulani zimepata maendeleo, zimepata pesa za kutosha, mabarabara ambayo ya kutosha. Lakini sehemu zingine zime kuwa ignored. Kwa hivyo lengo ya Jamhuri yetu itakuwa ni kuhakikisha kwamba maendeleo ni ya haki, kwamba yanafanyika na yanatekelezwa katika kila eneo la nchi.

Pia the role of science and technology: Kutumia science na maarifa ya elimu kuondosha disparities, kuondosha kutokuwa na usawa. Mwingine anaendelea zaidi kuliko mwingine. Na pia kumanaage National Resources fairly. Kuna mali ya asili, kuna mali ya uma. Mali ya asili ni kama vile wanyama wetu wa porini, dhahabu ikiwa iko, fedha ikiwa iko, diamonds na kadhalika, National Park, hizo ni mali za kiasili. Lakini pia kuna National Resources na Natural Resources. National Resources ni ile income tax inavyo ingia, mapato ya nchi kutoka kwa kila aina ya njia ambayo inakwenda treasury. Kwa hivyo Jamhuri yetu itahakikisha kwamba resources zetu, mali yetu, kila aina inatumiwa kwa njia ambayo ni ya uwadhilifu. Ili kila sehemu ya wananchi na kila sehemu ya nchi yenyewe inafikiwa na faida ya mali hiyo. Nafikiri kwa ufupi ni hayo ambayo ningependa kuhighlight katika chapter hiyo ya shabaha za Jamhuri yetu.

Chapter ya nne, ni citizenship: Hapa pia kumekuwa tumependekeza mambo tafauti kuliko hali ilivyo hivi sasa. Na mkisoma hapo wale ambayo muna ninino mutaona kwamba citizenship kwa kila mwananchi anahaki na ana duty au wajibu sawa na mwananchi mwenzake. Ikiwa mimi nina haki fulani singelazima awe nakama hizo not less. Mimi nikiwna wajibu wa kutimiza, wajibu pia, haki zinakwenda na wajibu. Wajibu wangu mimi lazima ni wajibu wake yeye. Hakuna mapendeleo kati yetu. Hiyo ndiyo principle ya muhimu ya wananchi.

Citizens are equally entitled to a Kenyan passport and to any document of identification issued by the State. Kila mwananchi anahaki ya kupata passport. Na conditions or masharti ya kupata passport kwa kile mmoja iwe ni ile ya mwenzake. Sio

mmoja anaambiwa wewe lazima in addition uwe na hivi na hivi na vile. Kama tujuavyo mambo hayo tumeyazungumza mara nyingi katika kukusanya maoni yenu. Tumepata malalamiko ya kwamba jamaa wengine wakienda kupata passport wanaambiwa leta pia na birth certificate ya nyanya yako na babu yako na kadhalika. Lakini mwingine haambiwi kufanya vile. That is discrimination. Kwa hivyo principles zilizoko hapa zimeondoa jambo kama hilo. The paper, the conditions for me should be the same for anybody else. All are going to be equal. Kisha tunaeleza jinsi ambavyo ni nani ambayo ni mwananchi.

Citizen by birth: Yeyote atakayezaliwa nchini Kenya ikiwa mzazi wake mmoja ni Mkenya basi huyo ni Mkenya automatically, si kwa kuzaliwa. Ikiwa baba ni Mkenya sio lazima mamake awe Mkenya. Every person born after coming into the Constitution is a Citizen of Kenya, if at the date of the person's birth either the mother or the father is a citizen of Kenya. Si lazima wote wawe ni Wakenya. Mama akiwa Mkenya mtoto awe ni Mkenya. Baba akiwa ni Mkenya lakini mama sio Mkenya pia ana haki ya uwananchi.

Kisha kuna citizenship and marriage. Hapo hawali kulikuwa na ubaguzi kidogo. Mama Mkenya au dada Mkenya, au mwanamke Mkenya akimuowa mtu wa ajinabi yule hapati na watoto wake huwa hawapati citizenship. Sasa ni sawa, wote wawili.

Citizenship by Naturalization: a person who has been a lawful resident in Kenya for a continuous period of not less than 7 years. Mutakikaa akishi Kenya kwa muda usiopungua miaka 7, huyo aweza kuapply kuwa Mkenya. Citizenship by Residence pia na kadhalika.

Chapter 5, kutakuwa na citizenship registration board. They will establish the citizenship registration board to deal with matters provided for under Act 27 consisting of not less than 5, and not more than 9 members appointed by the President with the approval of Parliament, from among persons of high moral standards. Body hiyo itashugulikia mambo haya. Ikiwa kuna mashtaka yoyote, malalamiko yote, body hii inaweza mtu anaweza kwenda kushtaki jambo lolote kuhusu wananchi.

Dual Citizenship: hili ni jambo jipya tumependekeza, amenikumbusha Silvia, sasa tunaruhusu kufuatia mswada huu wa Katiba kwamba mtu awe na haki ya kupata uwananchi zaidi ya nchi moja. Muhimu ni kwamba nchi hiyo ambayo mtu atakapopata wananchi wake iwe ni inchi ambayo inaruhusu dual citizenship. Kwa hivyo inasema Dual Citizenship is permitted under the laws of Kenya. A person who as a result of acquiring the citizenship of another country lost the citizenship of Kenya at any time before the coming into operation of the constitution is entitled on application to be registered as a citizen of Kenya. Yule ambayo alipoteza citizenship yake kwa kuwa alichukua citizenship nyingine kwanza huyo sasa aweza kurudi tena akawa citizen wa Kenya, au mwananchi wa Kenya. A person who loses Citizenship of Kenya as a result of acquiring the citizenship of another country is entitled on renunciation of the citizenship of that other country to regain that is the point I have just made. Sawa, yeyote ambayo hakufahamu anaweza kuuliza baadaye maana ni mswada mrefu na sitaweza kuwaeleza kwa kinaga naga kila jambo liloko.

Kisha chapter 5 au sura ya tano. Kuna the bill of rights ambayo ni muhimu sana. Kanuni ya haki. Haki ya kila aina. Kuna hiki wa kimsingi, kuna uhuru za kimsingi ambao kila mmoja wetu anahaki kuzipata. The Bill of Rights is the foundation stone of Kenya's Democratic State. Jiwe la msingi. Kanuni hii ya Bill of Rights ni jiwe la msingi, ukijenga jengo lolote lazima utie jiwego la msingi to (**inaudible**). The Bill of Rights is the foundation of Kenya as a Democratic State and is the framework for the adoption of social, Economic and cultural policies. Kufuatia kanuni hii, utajenga juu yake kila aina ya haki nyingine au siasa ambazo za mwathiri mwananchi katika kila sehemu. Inammwathiri hali yake kijamii, hali yake kiuchumi, hali yake kitamaduni na kadhalika.

Haki hizi, the Bill of Rights ni haki za kila mtu, na muhimu zaidi are not granted by the State. Ni haki ambazo umezaliwa nazo. Si haki ambazo umepewa na dola au na Serikali. ambayo kesho itakuambia nakupa haki hizi basi sasa nitakupokonya, la. They are inborn, ni haki yako tangu kuzaliwa na ambazo huwezi kunyanganywa tena. In alian rights, haki ambazo haziwezi ku...

Munajua hivyo pia Serikali ina wajibu, the State shall observe the respect, protect, promote and fulfill the rights and freedoms in this Bills of Rights. Si kulinda tu lakini kueneza haki hizo. Kutia moyo na kufanya kila jambo ili kila mtu apate haki zake. Na afahamishwe haki zake, ni wajibu wa Serikali kufanya hivyo. The State shall take reasonable legislative policy and other measures to achieve the progressive realization of the rights guaranteed in Act 56, 57,58,59,60,61 and 62. Ukisoma hii Katiba, articles hizo, vifungu hivo yinahusu zile basic needs tulizozitaja hapo awali. Haki ya kila mwananchi kupata chakula cha kutosha, matibabu ya kutosha, amani kwake yeye na jamii yake, elimu, makao, maji masafi na kadhalika. Kwa hivyo Serikali inawajibishwa na Katiba hii mpya au mswada wa Katiba hii kuhakikisha kwamba mambo haya yamekamilishwa na mwananchi atapata haki hizo.

Kuwatajia tu kijuu juu kuna right to life. Everyone has a right to life hakuna ambayo ana haki kuchukua roho au maisha ya mwenzake. Pia jambo lingine ambalo tumelifanya the death penalty is abolished. Hakutakuwa na adhabu ya kumtia kifo katika Kenya ikiwa mswada utakubaliwa.

Equality: haki ya usawa, kama nilivyo taja hapo awali, haki ya mtu kupata passport, birth certificate na kadhalika, ni haki ya kila mwananchi. Hapa every person is equal before the law and has a right to equal protection and equal benefit of the law.

Freedom from discrimination: haki ya kulindwa dhidi ya discrimination, ubaguzi. Hiyo ni haki.

Haki ya watoto: children (**inaudible**) it is the duty of their parents, wider families, society and the State to nurture, kuwalisha, protect, kuwalinda, educate them, kuwasomesha, so that they can develop in a safe and stable environment. In an atmosphere of happiness, love, respect and understanding, maybe able to fulfill their full potential in all respects. Nafikiri hiyo ni wazi.

Haki ya jamii au familia: the State shall recognize the family as the natural fundamental unit of society and has the necessary basis of social order.

Persons with disability, walemavu, haki zao: wanasisitizwa katika hii Bill of Rights kwa kila njia. Kwa upande wa elimu, kusahilisha maisha yao kwa hivi sasa wanapata taabu, hawana njia ya kupanda matatu hawezi, akitaka kupanda juu gorofa ya tatu hakuna lift, lazima apande kwa ngazi, na khadhalika. Ikiwa ni mtu ambayo hasikii ana taabu ya kusikia mambo yanayoelezwa. Ni kipofu hawezi kusoma hii Katiba ilivyoandikwa lazima aelezwe na mwingine. All these things will have to change. Lazima mabadiliko yafanywe ili kwamba walemavu wa kila aina, wanawezeshwa kushiriki katika maisha kama wenzao ambayo wemepata bahati ya kuwa hawana ulemavu wowote.

Human dignity: hii kwa uhakika ni sifa, taabu sana kuipin down. Human dignity ni mtu kuwa na sharafu yake. Bill of Rights inasisitiza kwamba kila mtu ana dignity yake ambayo Mungu amempa na lazima dignity hiyo, sharafu yake ile, iliendwe. Everyone has inherent dignity, amezaliwa na mtu ana sharafu yake, lazima mtu mwingine, mwenzake aiheshimu. The Right to have that dignity respected and protected.

Freedom and security of the person: awe amelindwa, vidi ya hatari yoyote, kwa njia yoyote. Ikiwa kuntaabu njiani, ghasia njiani, kuna violence ni wajibu wa wale ambayo wanashughulikia kuweka amani kumlinda kila mmoja wetu asifuatie na adhaa yeyote au hatari yoyote.

Not to be subjected to corporal punishment or to be treated or punished in a cruel, inhuman or degrading manner. Awe asiadhibiwe kwa njia ambayo ni ya kinyama, kama nilivyo sema hapo hawali mtu amezaliwa na sharafu yake. Inherent dignity, kumuadhibu, kumdhili, kumbadilisha, hiyo ni thidi ya Bill of Rights. Yeye au watu wake wanaweza kushtaki kuwa huyu ambadhibiwa kwa njia ya kinyama na hii ni thidi ya Constitution na yule aliye muathibu au kumjadilisha ataweza kustakiwa.

Slavery, servitude and forced labour: Mtu asilazimishwe, asifanywe mtumwa, mtu asilazimishwe kufanya kazi asiotaka kufanya yeye mwenyewe. Forced labour therefore is prohibited under the Bill of Rights na khadhalika.

.....Mwenyezi Mungu kwa njia ambayo yeye ataka kumuabudu na asilazimishwe kuhudhuria ibada ambayo yeye hataki kuhudhuria ya dini nyingine. Ikiwa ni mkristu asilazimishwe kuhudhuria ibada ya dini nyingine mwislaam pia asilazimishwe, mtoto wa kiswaam katika shule ambayo si ya kiswaam asilazimishwe kuhudhuria ibada ya dini nyingine, na khadhalika. Mutasoma kwa urefu zaidi jambo kama hilo.

To receive religious instructions or to take part in or attend a religious ceremony or to observe the day of rest of other observers that is not the person's religion. Yaani mtu kulazimishwa kufuata mila, dini na kusherekea siku ambayo ina

sherehekewa na dini nyingine na yeye analazimishwa kusherekea na khadhalika.

Freedom of expression: uwezo wa mtu kusema atakavyo. Awe na huru kusema bila kuogopa kwamba ataadhibiwa, atatiwa athabu, atafungwa na khadhalika. Lakini haki hii tuone kwamba pia ina mipaka yake. Ile haki yako ya kusema utakavyo isipite mipaka ukafikiria kwamba unaweza kutoa propaganda. Au kufanya jambo ambalo ni kama ni jambo la kivita, Mungiki vile kufanya haki yao ya kusema na kuteta, incitement, violence. Kuwahimiza watu kufanya jambo la kuvunja sheria na kupiga wenzao. Maana ukisema jambo ukatukana dini fulani, mathani, wale walioko katika dini hiyo ambayo umetukana wataudthika, sio? Hapa kutatokea na mapigano, vita na damu kumwagika. Mtu hanahaja kusema jambo, ana haja kusema atakavyo lakini ikiwa jambo lile ambalo atalisema litaleta hathari ya watu kupigana basi hiyo itakuwa si haki tena.

Advocacy of hatred that is based on discrimination and that constitutes the vilification of on others or incitement to cause harm. Propagation of all forms of prejudice. Kueneza ubaguzi wa kila aina. Ubaguzi wa dini, rangi, kabila na kahadhalika. Mtu atakaye toa maneno ambayo yatakuwa ni ya aina hiyo ya ubaguzi wa kirangi kutukana kabila fulani kwa kabila lile ni hivi, na vile au dini fulani ni hivi na vile, hiyo hairuhusiwi. That is not a right hiyo ni incitement to cause armed conflict or loss of life. Huenda ikasababisha watu kuuwawa au watu kuuliwa.

Publication of opinion: haki ya kuchapisha, access to information. Hivi sasa ukitaka kupata maelezo juu ya jambo fulani na khadhalika si rahisi kupata. Lakini sasa tunafikiria kwamba mwananchi sasa awe na haki ya kwenda kwokwote akasema nataka list ya watu ambayo ni hivi na hivi na vile kwa kuwa ninafanya kazi hino.

Tunataka tupate census sisi ni idadi gani ya watu katika District hii ya Mombasa. Na watoto ni wangapi, na akina mama ni wangapi. Walemavu katika Mombasa District ni wangapi. Kina mama ni wangapi? Inatakiwa ni haki yako kupewa habari hii katika zile wizara ambazo zinaweka maelezo kama hayo. Access to information ni jambo la muhimu sana. Maana mtu akipanga akitaka kufanya mipango ya maendeleo na khadhalika bila shaka atahitajia kila aina ya maarifa na information na itakuwa ni haki yake. Tuseme haki hii ya access of information ni haki ambayo hatuna hivi sasa lakini ukitimaza huu mswada wa Katiba mwisho kabisa kuna sixth schedule.

Wale ambayo wamekuwa wakinunua magazeti mutaona kwamba tulipo toa mswada wa Katiba hapo awali as a result of mistake kwa makosa tuliwacha sixth schedule au schedule no. six. Sasa hii sixth schedule ina mambo ambayo kuna haja ya kufanywa na Serikali. Ni muhimu kufanywa na Serikali ili kwamba hii Katiba iweze kutiliwa implementation. Kwa mfano right of access information tumesema time limit within which action shall be taken ni six months. Baada ya miezi sita Katiba hii mpya kutekelezwa au kutiwa iwe ni kanuni, lazima ile haki ya right to information iwe ishaanzishwa. Na baada ya hapo yeyote kati yetu akiwa na haja kujua jambo fulani, aweza kupata hiyo information atakayo.

Haki, Freedom of Association: mtu awe na haki kujiunga na chama chochote ambacho ni cha halali kama (**inaudible**) na

khadhalika.

Assembly, demonstration, picketing and petition: mtu ana haki kupeleka mashtaka yake akitaka, petition yake popote katika wizara yoyote kwa njia ambayo bila shaka itaelezwa baadaye. Pia haki ya kupicket, kusimama nje ya Municipal Council, nje ya uhuru na kazi, kuwazuia wale ambayo wako katika Union yako wasiendeleo na kazi. Hiyo ni haki inayofuatwa katika nchi nyingine, ili mashtaka yako yapate kuwa na umoja na wenzako kufuatia...

Political Rights: demonstration pia unahaki. Maadam demonstration ni ya kiamani unahaki ya kudemonstrate hakuna ambayo anaweza kukuzuiya. Political Rights unahaki to make political choices kama nilivyo sema kujiunga na chama chochote cha kisiasa. Hakuna atakaye kulazimisha kujiunga na kile ambcho yeye ataka uungane nacho.

Freedom of movement and Residence: every person has a right to freedom of movement. Hakuna atakaye kuzuia usitoke Kenya, usitoke Mombasa na kahadhalika. Pia everyone has the right to leave the Republic. Hakuna atakaye kuzuiya airport kukuambia usitoke. Every citizen has a right to enter into the Republic. Una haja ya kurudi, umetoka ukazuiliwa airport huwezi kuingia ikiwa wewe ni mwananchi una citizenship hakuna atakuwa na haki ya kukuzuia kurudi nchini na khadhalika.

Refugees and Asylum: freedom of trade, occupation and profession. Una haja ya kufanya hijara au biashara yeyote utakayo na khadhalika. Haki ya kumiliki jambo lolote maadam ni malie ya halal. Unahaki ya kuimilikia.

Haki ya Social Security: huwezi kulazimishwa kusema wewe ni kabila gani (**inaudible**) ni nini. Hii ni kuondoa mambo iliomo katika forms zingine ambazo tuwaziona saa zingine kwamba jina lako ni nini? Umri wako ni ngapi? Kabila lako ni kabila gani? Na khadhalika. Tunataka kuondoa mambo yote kwamba mtu ni mwananchi tu. Hakuna ambayo atalazimishwa kusema mimi ni Mluhya, mimi ni Mwamu, mimi ni Mbajuni, mimi ni Mdigo na khadhalika, hiyo si lazima tena, haina haja. A citizen is a citizen, tuache mambo hayo ya ukabila na mambo ya kusema huyu ni mwislaam, huyu ni Mkristu, huyu ni kadhalika

Pia yule atakaye shitakiwa anahaki pia. Every person who is arrested for allegedly committing an offence has a right to remain silent. Hii ni sheria ambayo inatumiwa kule Europe hivi sasa kwa muda mrefu. Maana yake hana maarifa ya kanuni. Asije akasema jambo akajitia katika kitanzi. Kwa hivyo na aweze kunyamaza kimya, mimi siwezi mpaka ni mpate wakili wangu. Na aweza kuremain silent, abakie kimya mpaka wakili wake atakapokuja ambayo atamtetea. Na kila mmoja ana haki ya kuelezwa ameshitakiwa kwa jili ya jambo gani. Kwa lugha ambae anaifahamu pia. Na haki zingine zilizoko. Pia yule ambaye atashikwa leo asiwekwe na wale ambayo tangu hapo wako kwenye jela, awe mbali na hayo. To be brought before the court as soon as possible but not later than 48 hours of being arrested. Ataletwa mbele ya mahakama isichelewe zaidi ya masaa arubaini na nane. Akiwekwa zaidi ya hivyo ni (**inaudible**) ya kanuni. Tunajua kwamba wengine saa zingine wanashikwa wanakaa siku mbili, tatu, inne hajatolewa. Kwa hivyo mambo kama haya ambayo malalamiko mengi tumepata katika kuzunguka hapa na pale. Wengi wanashitaki kwamba watoto wao au ndugu zao na khadhalika au jamaa zao wanashikwa wanakaa indefinitely,

bila kupelekwa mbele ya korti. Fair trial, Rights of persons highly held in custody pia.

Chapter six: Representation of the people - mambo ya Bunge na election na Khadhalika, yameelezwa kwa kinaganaga kirefu.

Mambo ambayo ningetaja hapa ni machache tu.

